

# Uchaguzi



- ☑ Raia wa Marekani watapigana kura ya kumchagua Rais wa Marekani na maafisa wengine wanaochaguliwa mnamo tarehe 5 Novemba, 2024. Siku hii unaweza kuona mistari mirefu ya watu wanaosubiri kupiga kura. Upigaji kura unafanyika kwenye sehemu za umma au zinazosimamiwa kama vile shule, vituo vya zimamoto na makanisa.
- ☑ Hadi kufikia Siku ya Uchaguzi, unaweza kupokea ujumbe wa kisiasa au kupigiwa simu au watu wa kampeni kubisha hodi mlangoni mwako. Huna haja ya kujibu uhumbe huu.
- ☑ Tafadhali kumbuka kwamba ikiwa wewe si raia wa Marekani, huenda usipige kura wala kujisajili kwa ajili ya kupiga kura, na kwa kufanya hivyo kunaweza kuwa na madhara makubwa sana, ikiwa ni pamoja na kupoteza hadhi yako au kukabiliana na kufurushwa nchini.
- ☑ Wamarekani wana hisia kali sana kuhusu mgombea wao wa Urais (Donald Trump au Kamala Harris). Unaweza kuona mikusanyiko mikubwa ya watu wakionesha kumuunga mkono mgombea wao kabla au baada ya uchaguzi.
- ☑ Unaweza kuona watu wengi wakiwa wamekusanyika ili kuandamana au kusherehekea. Tafadhali chukua tahadhari kuwenye mikusanyiko mikubwa.
- ☑ Ikiwa utaamua kuandamana tafadhali usiende peke yako na chukua vitu vifuatavyo: barakoa, maji, kitambulisho, kitakasa mikono, na namba za simu ya dharura.
- ☑ Ikiwa utahisi kuwa upo hatarini au wewe ni mhanga wa vitendo vya kutumia nguvu, tafadhali piga simu kwenye namba 911. Mara baada ya kuwa katika sehemu salama, tafadhali wasiliana na IRC ili tuweze kukupatia usaidizi wa ziada au kukusaidia kuripoti polisi.